## Kusoma Zaidi

# Upatanisho wa kisarufi.

Upatanisho wa kisarufi katika ngeli za nomino hujitokeza pale ambapo nomino zikitumiwa katika sentensi, sharti kuwe na upatanisho fulani ili kuhakikisha kwamba sentensi inakubalika kisarufi. Kila ngeli huwa na upatanisho wake ili kuhakisha kuwa sentensi ni sahihi kisarufi. Upatanisho huu unadhihirika kwa kutumia viambishi fulani ambavyo huitwa **viambishi vya upatanisho wa kisarufi.** Kila ngeli huwa na viambishi ambavyo hutumiwa ili kuhakikisha kuwa sentensi ni sahihi.

Katika mifano ya sentensi iliyotolewa hapo juu, nomino zilizotumiwa ni za ngeli mbalimbali katika umoja na wingi. Viambishi vilivyokolezwa rangi ni vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli husika. Usahihi wa sentensi hutegemea matumizi ya viambishi hivi katika sentensi.

Wakati wa kutambua nomino inapatikana katika ngeli gani, upatanisho wa kisarufi unaweza kumwelekeza mwanafunzi kwa kuzingatia viambishi vilivyotumiwa. Ni muhimu kuzingatia kwamba, umbo la nomino katika ngeli hutofautiana kwa wakati mwingine. k.m. nomino katika ngeli ya KI-VI katika umoja huwa zinatofautiana.

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| a) Kitabu | Vitabu |
| b) Chakula | Vyakula |
| c) Cheo | Vyeo |
| **d)** Kiatu | Viatu |